

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji [W])

WILAYA YA BAGAMOYO:

Simu: 023 - 2440164

Fax: 023 – 2440338



**OFISI YA MKURUGENZI
MTENDAJI (W)
S.L.P. 59,
BAGAMOYO
MKOA WA PWANI**

Email: ded.bagamoyo@pwani.go.tz

Kumb.Na.HWB/A.20/75/135

10/10/2017

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inapenda kuwatangazia Mafundi wote wenye sifa ya kuomba nafasi ya kazi ya ujenzi wa kituo cha Afya Kerege-Majengo manne(4) ambayo ni wodi ya akina mama, jengo la upasuaji, jengo la maabara na nyumba ya mtumishi.

1. Fundi ujenzi -Nafasi 4

2. KAZI NA MAJUKUMU

- Kusimamia ujenzi / atakuwa ndiye Fundi mkuu katika jengo husika.
- Atakuwa tayari kupokea na kuzingatia maelekezo ya mhandisi
- Atahakikisha michoro na maelekezo Vinafuatwa wakati* wa ujenzi

3. SIFA ZA ZINAZOHITAJIKA:

- Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha IV/VI aliyehitimu mafunzo ya ufundi stadi veta grade I au level III; mwenye cheti cha ufundi sanifu (FTC) atafikiriwa zaidi.
- Uzoefu usiopungua miaka mitatu katika kazi za ujenzi.(ambatanisha wasifu(CV)
- Uwezo wa kutafsiri michoro mbalimbali

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBALI WOTE AMBAYO NI LAZIMA KUZINGATIWA:

1. Mwombaji ni lazima awe ni Raia wa Tanzania.
2. Barua ya maombi ni lazima iambatanishwe na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni na kuitishwa kwenye ofisi ya serikali ya mtaa au kata. **Pamoja na wasifu (CV) kwa wasimamizi wa ujenzi**)

3. Awe na umri wa zaidi ya miaka 18 na usiozidi miaka 45.
4. Awe na akili timamu na Afya njema.
5. Maombi yote yaletwe kwa mkono na kuwasilishwa katika ofisi za masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Bagamoyo.
6. Usaili utafanyika tarehe 17/10/2017 kuanzia saa 3.00 asubuhi
7. Barua za maombi zitumwe kwa; anuani ifuatayo

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO,
S.L.P. 59,
BAGAMOYO

8. Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 16/10/2017 saa 6:30
Mchana.



CHARLES R. WAMBURA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO *MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA*
BAGAMOYO

Nakala

- 1) Katibu tawala (W)
- 2) Ofisi za watendaji kata halmashauri ya wilaya bagamoyo
- 3) Ofisi ya Mganga mfawidhi zahanati ya kerege
- 4) Mbao zote za matangazo za Halimashauri

NB: TANGAZO HILI PIA LINAPATIKANA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI
www.bagamoyodc.go.tz